Ofisi ya Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa

Hotuba ya Mwenyekiti Mwenza wa Kundi la Washirika wa Maendeleo na Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania
Alberic Kacou
Mazungumzo ya Mwaka kuhusu Sera ya Taifa
26 Januari 2012

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mizengo Kayanza Pinda
Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mustafa Mkulo
Waheshimiwa Mawaziri,
Waheshimiwa Wabunge,
Makatibu Wakuu,
Mabalozi na Wawakilishi wa Nchi,
Maofisa Waandamizi katika Serikali ya Tanzania,
Wakuu wa Mashirika ya Ushirikiano,
Wawakilishi wa Asasi za Kiraia,
Waandishi wa Habari,
Wageni Mbalimbali,
Mabibi na Mabwana,

Kwa niaba ya Kundi la Washirika wa Maendeleo, ningependa kuwashukuru nyote kwa kuja kwenu na ninawatakia heri na fanaka za mwaka 2012. Kwa kweli ni heshima kubwa kuhutubia mkusanyiko huu wa hali ya juu unaowaleta pamoja watu wenye ushawishi mkubwa na wenye uelewa mpana. Mazungumzo ya Mwaka kuhusu Sera ya Taifa ni mkutano muhimu katika kalenda ya Tanzania kwa sababu yanawaleta pamoja wadau wakuu katika mchakato wa maendeleo ya taifa ili kujadili – kwa njia za mashauriano na uwazi – kuendelea kuimarisha juhudi za kupunguza umaskini na kukuza uchumi kwa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo ya taifa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Katika Mkutano wa Mwaka kuhusu Sera ya Taifa uliofanyika kwa mara ya mwisho mwaka 2010, tulikaribisha majadiliano motomoto kuhusu MKUKUTA awamu ya II na MKUZA awamu ya II. Hivi sasa tunatarajia kuona ukamilishaji wa vipengele vitatu vya nyongeza kwenye MKUKUTA awamu ya II: mpango wa utekelezaji, mkakati wa mawasiliano, na muundo wa usimamizi na tathmini (M&E).

Kazi iliyokwishafanyika kuhusiana na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ni ya kutia moyo na ni hatua kubwa kwa Tanzania inayolenga kuimarisha uelekezaji madhubuti wa mikakati kwenye malengo ya Visheni ya Mwaka 2025 ili kuhakikisha upatikanaji wa maisha bora zaidi na nchi kuvuka na kuingia katika hadhi ya kipato cha kati. Washirika wa Maendeleo wanayo furaha kuona kwamba uwasilishaji wa Mpango huo umepewa nafasi ya kutosha kwenye programu hii. Majadiliano ya kina ya leo bila shaka yatatoa mang'amuzi zaidi kuhusu ni kwa jinsi gani Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unahusiana na MKUKUTA awamu ya II kwa maana ya uwekaji vipaumbele, utoaji fedha na mpangilio wa shughuli za maendeleo.

Kwa mantiki hii, uwiano kati ya ukuaji wa kiuchumi, mikakati kwa ajili ya ugawaji mpya wa rasilimali na sera zinazolenga kuwasaidia maskini ni masuala muhimu hasa kama tunataka, katika miaka ijayo, kuhakikisha kuwepo kwa ukuaji jumuishi ambao unatoa nafasi kwa takribani Watanzania milioni 12.9 ambao kwa mujibu wa Taftishi ya Bajeti ya Kaya ya Mwaka 2007 wanaishi katika umaskini. Huku idadi ya watu duniani ikiwa imeshavuka watu bilioni 7, kupata na kutumia rasilimali linazidi kuwa jambo muhimu, hasa katika nchi kama Tanzania ambamo kasi ya ukuaji idadi ya watu ni ya juu. Sote kwa pamoja, kwa hiyo, tunakabiliwa na changamoto ya msingi ya kuhakikisha kwamba mikakati ya kimaendeleo tunayoweka inalenga idadi ya watu inayokua kwa kasi, kwa namna iliyo endelevu na inayoleta ustawi wa kiuchumi kwa Watanzania wote.

Wakati ambapo Tanzania imepata ukuaji wa kuridhisha katika muongo uliopita, katika wastani wa asilimia 7, bado kuna uwezekano wa kuongeza kasi hiyo hata iingie kwenye wastani wa makumi, hatua ambayo itakuwa na nguvu sana dhidi ya kupunguza umaskini. Jambo hili litamaanisha kufanya uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu, sekta za kijamii na vilevile kuhakikisha mazingira madhubuti ya uchumi mpana kupitia sera bora za fedha na usimamzi wa masuala ya fedha.

Vilevile, dhima ya sekta binafsi katika kutoa ajira na kuendeleza ukuaji nchini Tanzania ni muhimu sana. Ingawa changamoto zingalipo, kumekuwa na kupiga hatua kwa upande wa Mpango wa Serikali wa Mazingira ya Uwekezaji ili kushughulikia vikwazo muhimu katika mazingira ya kibiashara, hasa katika kuimarisha mipango ya kitaasisi ili kuleta mageuzi. Hata hivyo, Mpango huo ni mpana kama ilivyoainishwa katika Faharasa za Ufanyaji Biashara na Ushindani wa Kidunia za mwaka 2011/2012. Mageuzi yenye kasi kubwa katika Mpango wenye klasta nane ni muhimu ili kuhakikisha kwamba Tanzania inaendana na kasi ya washindani wake. Ufumbuzi wa muda mrefu unaolenga kuwepo kwa uzalishaji nishati ulio endelevu utasaidia kuifanya nchi iweze kushindana katika chumi za kikanda na ulimwengu.

Ndugu Wageni Waalikwa,

Ni jambo linalostahili kutambuliwa katika majadiliano ya leo na kesho kwamba Tanzania imekuwa na mwelekeo chanya wa ukuaji katika kipindi cha miaka mitano iliyopita katika kuimarisha utendaji wake kwenye Maendeleo ya Watu. Tanzania, kwa kulinganisha na nchi nyingine, inaendelea kubaki kuwa ndiyo nchi inayofanya vema sana katika ukanda Kusini mwa Jangwa la Sahara. Licha ya maendeleo haya ya kutia moyo, bado kuna changamoto za kutosha zinazohusiana na kupunguza umaskini. Kwa kutumia lugha ya Faharisi ya Maendeleo ya Watu (HDI), asilimia 65 ya Watanzania wanaishi katika kile kinachoitwa 'umaskini wa pande nyingi' huku wakiwa na fursa chache za elimu, afya, maji salama na safi, usafi, umeme, nishati ya kupikia na mali. Ni jambo muhimu sana kwamba Serikali na washirika wake wa maendeleo wafanye juhudi zaidi ili ukuaji huo makini wa kiuchumi ambao Tanzania imekuwa nao katika muongo mmoja uliopita, ujidhihirishe kwenye viwango vya kupungua kwa umaskini, upatikanaji wa elimu bora zaidi na upatikanaji wa huduma bora zaidi za maji na afya.

Kwa hiyo, juhudi za kuleta usawa zaidi wa kijinsia na uwezeshaji wanawake hazina budi kuongezewa kasi, kwa kutambua kwamba haya ndiyo maeneo muhimu ya kupata matokeo hayo ya kimaendeleo. Kupunguza kukosekana kwa usawa wa kijinsia lenyewe ni lengo na vilevile ni sharti muhimu kwa ajili ya ukuaji unaolenga maskini ulio endelevu na jumuishi.

Kwa zaidi ya muongo mmoja, hatua muhimu za kukuza uwezo na ufanisi wa Serikali katika utekelezaji zimehusishwa na mabadiliko ya msingi kama vile Maboresho ya Serikali za Mitaa na Maboresho ya Utumishi wa Umma. Ugawanyaji madaraka ulio

kamilifu na unaolenga matokeo katika taasisi za serikali ni muhimu ili kupanua na kueneza huduma za umma, hasa katika maeneo ya vijijini. Jambo hili linahusu huduma kama vile afya hasa kwenye maeneo yenye viwango vya juu vya vifo ya akina mama, au elimu ya msingi katika hali ambapo viwango vya ufaulu vinazidi kushuka. Manufaa ya nyongeza, bila shaka, ni uimarishaji umiliki mahalia na uwazi katika mchakato wa maendeleo katika ngazi ya wilaya. Kiwango hichohicho cha umakini kielekezwe kwenye Maboresho ya Utumishi wa Umma na utekelezaji wa Sera ya Malipo katika Muda wa Kati kupitia mkakati unaomudu kwa ufanisi kabisa ili kuhakikisha kuwepo kwa mgawanyo wenye uwiano wa rasilimali watu katika sekta zinazotoa huduma kwenye maeneo yaliyosahaulika.

Maendeleo makubwa yanayostahili pongezi yamefanyika katika kuzingatia suala la mabadiliko ya tabia ya nchi na mazingira katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, huku kukiwa na mwelekeo madhubuti zaidi wa kushughulikia siyo tu dhima yao ya kimkakati katika ukuaji na maendeleo, lakini pia uwezo-tuli wao wa kuhamasisha vyanzo vingi zaidi vya fedha. Kadiri Tanzania inavyojielekeza kujipatia fedha kutoka vyanzo vya ulimwengu kwa ajili ya mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi kupitia uendelezaji wa muundo wa kitaasisi kwa ajili ya ufanisi katika kuhimili mabadiliko ya tabia ya nchi, vilevile itakuwa muhimu kuhakikisha muundo wa utumiaji unashughulikia usimamizi wa mali asili za taifa zenye kuzalisha kama vile maji, misitu na uvuvi.

Mabibi na Mabwana,

Mfuko (chombo) wa Misaada ya Jumla ya Bajeti (GBS) bado unaendelea kupendelewa kutumiwa kama njia ya misaada kwa Serikali ya Tanzania. Kupitia chombo hiki, Washirika wa Maendeleo 12 wanatoa msaada wa kifedha moja kwa moja kwenye bajeti ya taifa ya shughuli za maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Chombo hiki kimewekwa ili kuendana na vipaumbele vya taifa, hutumia mifumo ya kitaifa na huipatia Serikali udhibiti kamili wa ajenda yake ya maendeleo huku ikitia msisitizo zaidi kwenye uwazi na uwajibikaji wa Serikali.

Uongozi madhubuti wa Serikai wa chombo hiki cha GBS na mzunguko wa mwaka wa tathmini ulijidhihirisha wazi zaidi mwaka 2011, ambapo Serikali iliongoza maandalizi na utekelezaji wa moja ya Mapitio ya Mwaka ya GBS yaliyokuwa yenye mafanikio zaidi kuwahi kuonekana nchini Tanzania. Wakati ambapo Serikali na washirika wake

wa GBS walifaulu kukubaliana katika vigezo vyote vya tathmini – hata vile ambavyo huwa na changamoto nyingi – bado, hata hivyo, kuna haja ya kuleta matokeo yaliyo wazi zaidi na yenye matokeo yanayoonekana katika ushirikiano na GBS.

Changamoto kubwa kwa nchi yoyote duniani ni kushinda vita dhidi ya rushwa. Jambo hili pia linaihusu Tanzania. Kwa hiyo, hatua za uwazi, uwajibikaji na kupiga vita ufisadi ni muhimu kwa ushirikiano wa maendeleo wenye ufanisi, kwa ajili ya kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja, kwa kuweka nafasi kwa ajili ya maendeleo ya sekta binafsi, na kwa kuongeza ubora katika upatikanaji wa huduma za msingi za jamii. Washirika wa Maendeleo wanakaribisha utayari wa kisiasa wa uongozi wa Tanzania katika kuongeza nguvu katika vita dhidi ya ufisadi, iwe kwenye kesi zinazohusisha watu wazito serikalini na hata kwa zile rushwa zinazoitwa za uchwara hasa katika sekta fulani fulani, zikiwemo zile za afya, polisi na mahakama.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Ni muhimu pia kutambua kwamba Tanzania ni moja ya nchi ambazo zimekuwa mstari wa mbele kwa miaka mingi kutetea ajenda ya ufanisi wa misaada. Pale Jukwaa la Viongozi Waandamizi lilipofungwa mnamo Desemba 1, 2011, ilikuwa ndiyo mwisho wa mchakato wa miaka minane ulioanza Roma mwaka 2003, na ambao ulipanuliwa sana mwaka 2005 jijini Paris na tena mwaka 2008 jijini Acra. Ingawa vipengele vya utekelezaji vya Tamko la Busan bado havijakamilishwa, baadhi ya vifungu vilivyo bayana kwa ajili ya masuala ya misaada kwa siku za usoni vimeibuka:

- **Kanuni za Paris na maeneo ya vipaumbele yanabaki kuwa lengo letu, hata hivyo kwa kuweka msisitizo zaidi kuhusu uwazi na uwajibikaji kuliko hapo kabla.**
- **Serikali na Washirika wa Maendeleo hawana budi kushughulikia masuala na maboresho yaliyokubaliwa Paris na Accra na ambayo yalikuwa bado kukamilishwa.**
- **Na lililo muhimu kuliko yote: Hatuna budi kufikiri zaidi ya njia za upatikanaji misaada tulizozizoea. Tunavyoshiriki kwenye mazungumzo haya leo, wadau wote hawana budi kushiriki kwenye dhima muhimu katika juhudi za maendeleo za taifa. Katika mantiki hii, maendeleo si tu kwamba yamefungwa kwenye umiminikaji wa misaada kutoka Washirika wa Maendeleo, bali inazidi kuhusishwa kwenye wigo mpana zaidi wa nyenzo za usimamiaji fedha na ushirikiano kama vile:**

- **Vyanzo vya ndani kutoka kwa raia;**
- **Uwekezaji wa moja kwa moja kutoka ndani au nje kupitia sekta binafsi;**
- **Raia walio ughaibuni;**
- **Ushirikiano wa Nchi za ukanda wa Kusini;**
- **Asasi za Kiraia za hapa nchini na zile za kimataifa;**
- **Mikopo ya kimataifa;**
- **Mshirika asiye mwanachama wa DAC kama vile Brazili, China, India na Afrika ya Kusini;**
- **Utoaji fedha kwenye vyanzo mbalimbali ulimwenguni;**
- **Na vilevile, fedha za ndani kwa ndani kwenye taasisi, asasi na misingi, hiyo ni kwa kutaja tu mifano michache.**

Tayari Tanzania imekwishatekeleza nyingi kati ya Kanuni za Paris. Licha ya hilo, bado kuna nafasi ya kusonga mbele, hasa katika kuanzisha muundo wa uwajibikaji na unaolenga matokeo ulio wazi zaidi na ambao unaweza kuongoza ushirikiano kati ya Serikali na wadau wake wa kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu,

Kwa kumalizia, kwa hakika siku za usoni zina neema nyingi kwa nchi ya Tanzania. Viwango vya ukuaji ni vya kuridhisha, hata katika kipindi hiki ambapo jumuiya ya kimataifa ipo kwenye kilele vya migogoro ya kifedha. Majadiliano na fikra kuhusu uwekaji vipaumbele kimkakati kuhusu ajenda ya maendeleo bado yanaendelea kujikita kwenye jambo hilo, ambalo ni jambo muhimu katika kulenga maeneo ambayo uwezekano wa ukuaji zaidi unaweza kuchochewa. Utafutaji fedha hapa nyumbani kwa ajili ya maendeleo ya kitaifa unaweza kupanuka katika miongo ijayo hasa Tanzania inavyoanza kufanya upembuzi wa gesi, mafuta na rasilimali nyingine. Mkazo wetu uwekwe kwenye kuhakikisha kwamba sera zinazotekelezwa leo zifungue milango kwa siku za usoni na kutoa hakikisho kwamba kunakuwa na ustawi wa Watanzania wote, hasa wale walio maskini na dhaifa zaidi. Kwa hiyo, hatuna budi kupambano kwa ajili ya hapa:

- **Kwanza, kuunda ushirika ambao unalenga kusaidia visheni ya maendeleo ya Tanzania katika njia ya kimkakati inayojenga juu ya maendeleo yaliyokwishapatiakna katika miongo iliyopita na kuingiza maeneo mapya kama**

vile kuongezeka kwa idadi ya watu na mabadiliko ya Tabia ya Nchi katika kuongeza kasi ya juhudi za maendeleo yaliyo endelevu;

- **Pili, kutambua kwamba sisi sote, kama washirika hatuna budi kushiriki dhima pana zaidi katika kupunguza umaskini kwa kuunganisha nguvu, ujuzi na weledi wetu uliotawanyika katika maeneo mengi;**
- **Tatu, kufanya juhudi ili kupanua na kuongeza umiliki na uongozi wa kitaifa katika suala la ajenda ya maendeleo pamoja na wadau wote wanaohusika katika namna iliyo ya wazi, kuwajibika na inayolenga kuleta matokeo.**

ASANTENI SANA